# HAKI ZA KIRAIA NA FOMU LA KUIDHINISHA– SAMPULI YA USHAHIDI YA ☐ PUMZI AU ☐ DAMU

(Chagua Moja)

Mfungwa:______________________________________________________Tarehe: ___________________________

Mfungwa alishauriwa kuhusu yafuatayo (Sehemu za 1 – 10):

1. Umefungwa kwa makosa ya Kuendesha Gari Ukiwa Umelewa na unahakikishiwa uwepo wa haki fulani.
2. Utaruhusiwa kutumia simu ikiwa unajigharamia ili kuwasiliana na familia au marafiki wako, kupangia kuachiliwa kwa dhamana, au kuajiri wakili. Matumizi hayo ya simu yanaweza kuhairishwa hadi idhini au kukataa wako umeandikwa kwenye fomu hii. Bila kujali haya, kutumia kwako kwa simu kutakubalika ndani ya saa moja ya kuwasili kwako.
3. Una haki, ukiomba na ukigharamia, kukaguliwa moja kwa moja na daktari utakayochagua. Utapatiwa fursa iwezekanavyo kutumia haki hii, lakini mchakato wa kipimo hautacheleweshwa ikingoja ukaguzi huu.
4. **Ninaomba utoe idhini kwa ☐ kipimo cha ushahidi cha pumzi / ☐ kipimo cha ushahidi cha kutoa damu na kupima *(chagua moja)* ili kuhakikisha kiwango cha pombe katika damu yako.**

   Viwango vifuatayo vinahusu haki yako ya kuendesha gari:
5. Madereva CHINI YA Miaka 21: Ukikataa kipimo hiki, leseni yako ya kuendesha gari ndani ya Massachusetts itaghairiwa kwa muda wa miaka 3 hadi maisha yako yote. Iwapo kiwango cha pombe katika damu yako ni .08 au juu zaidi, umekiuka sheria za Massachusetts na unaweza kupata mashtaki ya jinai. Iwapo kiwango cha pombe katika damu yako ni .02 au juu zaidi, Idara ya Usajili wa Magari itaweka faini ya kiusimamizi dhidi yako. Iwapo utachukua kipimo hiki halafu ufeli, muda wa kughairi leseni yako ni masiku 30, lakini pia utakabili kughairiwa kwa muda wa ziada wa masiku 180 na hadi mwaka 1 na Idara ya Usajili wa Magari.
6. Madereva Wenye Miaka 21 au ZAIDI: Iwapo utakataa kipimo hiki, leseni yako au haki ya kuendesha gari katika Massachusetts itaghairiwa kwa muda wa masiku 180 hadi maisha yako yote. If your kiwango cha pombe katika damu is .08 au juu zaidi, umekiuka sheria za Massachusetts na unaweza kupata mashtaki ya jinai. Ukifanya kipimo na kiwango cha pombe katika damu yako ni .08 au juu zaidi, basi muda wa kughairi ni masiku 30.
7. Ukiamua kufanya kipimo, utakuwa na haki ya kufanya kipimo cha kulinganisha cha damu ndani ya muda mwafaka kwa gharama yako. Matokeo ya kipimo linganishi la damu linaweza kutumika kupata upya leseni yako au haki ya kuendesha gari katika kusikiliza kesi mahakamani ndani ya masiku 10.
8. Kukataa au kukosa kutoa idhini ya kuchukua kipimo hiki cha ushahidi ni kukiuka Sheria ya Haki ya Kutoa Idhini na itasababisha ughairi wa haki yako ya kuendesha gari. Kukataa kipimo hiki na kuomba aina nyingine ya kipimo kinaamuliwa kuwa kukataa chini ya sheria hii.
9. Zaidi ya hayo, iwapo unamiliki Leseni ya Dereva wa Kibiashara (CDL) au usipomiliki leseni hii, mtu yeyote atakayekosa kukubali kipimo hiki atakosa haki ya kuendesha gari ya kibiashara kwa muda wa mwaka 1 hadi maisha yote.
10. Iwapo ulikuwa unaendesha gari inayosafirisha vitu hatari inayotakiwa kuwekwa mabango, kukosa haki wa kuendesha kwa CDL iliyosababishwa na kukataa kipimo utakuwa wa hadi miaka 3. Iwapo ulifungwa hapo awali kwa makosa inayofanya ukose haki inayoelezewa ndani ya sheria za serikali shirikisho za CDL au sheria ya eneo, kukosa haki hiyo ya kuendesha ya CDL itakuwa kwa maisha yote.

**Baada ya kushauriwa na kufahamu yaliyo hapa juu, je unatoa idhini kwa kufanya**
**☐ kipimo cha ushahidi cha pumzi / ☐ kipimo cha ushahidi cha kutoa damu na kupima (*chagua moja*)**
**Ambayo ninaomba kufanya ili kuhakikisha kiwango cha pombe katika damu yako?**

**☐ Ndiyo ☐ Hapama Wakati wa Kutoa Idhini au Kukataa ________**

**Nimesoma na nimefahamu Fomu hii ya Haki za Kiraia na Kutoa Idhini.**

**Saini ya Mfungwa:** ________________________________________________ **Tarehe** ____________________

**Saini ya Afisa wa Kumfunga au Mtekelezi wa Kipimo cha Pumzi:** ______________________________ **Tarehe** ____________________

**Saini ya Shahidi wa Kukataa:** ________________________________________ **Tarehe** ____________________
**(Ni lazima iwe tofauti na afisa aliyetia saini hapa juu)**

---

**HAKI KWA DAKTARI** Sheria Kuu, Ch. 263, Sec. 5A: Mtu aliye chini ya ulinzi wa kituo cha polisi au sehemu nyingine ya kufungwa, aliyeshtakiwa na kuendesha gari huku amelewa, atakuwa na haki, akiomba na akigharamia, kupimwa mara moja na daktari atakayemchagua yeye. Afisa wa polisi anayesimamia kituo hicho au mahali amefungwa, au mwakilishi wake, atamjulisha kuhusu kuwepo kwa haki hiyo mara moja baada ya kusajiliwa kufungwa, na atampatia mfungwa fursa mwafaka ya kutumia haki hiyo. Mfungwa huyo, mara moja baada ya kusajiliwa kufungwa, atapatiwa nakala ya sehemu hii ya sheria isipokuwa iwapo nakala kama hiyo inapatikana katika kituo cha polisi au sehemu aliyefungwa katika eneo ambapo inaonekana na ambapo mtu huyo anaweza kuipata.

**HAKI YA KUTUMIA SIMU** Sheria Kuu Ch. 276, Sec. 33A: Afisa wa polisi anayesimamia kituo hicho au mahali amefungwa ambapo mtu huyo ako chini ya ulinzi, atamkubali atumie simu inayogharamiwa na mfungwa, ili kumkubalia mfungwa awasiliane na familia au marafiki wake, au kupangia kuwachiliwa kwake kwa dhamana, au kuajiri wakili. Mtu kama huyo atajulishwa moja kwa moja baada ya kuwasili katika kituo hicho au sehemu cha kufungwa, kuhusu haki yake ya kutumia simu, na matumizi ya simu yatakubaliwa ndani ya saa moja baadaye.